



**08/Januari/2025.**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KUTOKA KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD.**

KCU (1990) LTD, ni chama kikuu cha ushirika mkoa cha Kagera kinachohudumia wilaya tatu ambazo ni Bukoba, Muleba na Misenyi. Kinatangaza ajira kwa nafasi zifuatazo:

**MHASIBU MKUU 'CHIEF ACCOUNTANT' (NAFASI 1).**

**VIGEZO NA UZOEFU.**

- I. Awe na Shahada ya kwanza katika masomo ya uhasibu, fedha na utawala wa biashara kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- II. Lazima awe na taaluma ya 'CPA' katika daraja la 'Associate/Fellow'
- III. Awe na walau uzoefu wa miaka mitatu katika kazi ya uhasibu.
- IV. Awe na uwezo wa kushirikiana na wenzake katika kutimiza malengo ya taasisi.
- V. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta pamoja na Mifumo ya TEHAMA.
- VI. Awe na umri wa kuanzia miaka 25 na kuendelea.
- VII. Awe ni raia wa Tanzania.
- VIII. Awe hajawahi kuhukumiwa kwa kosa la jinai.

## **MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO.**

- (i) Mshauri Mkuu wa Meneja Mkuu, Menejimenti na Bodi ya Chama kuhusiana na masuala yote ya fedha;
- (ii) Kusimamia idara ya Uhasibu na kufuatilia taarifa za fedha kila siku;
- (iii) Kuhakikisha kwamba kazi za kifedha za KCU zinatekelezwa kwa usahihi na kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa;
- (iv) Kuratibu zoezi la uandaaji bajeti.
- (v) Kuhakikisha kwamba marejesho yote ya kisheria yameandaliwa na fedha zinazotumwa zinatolewa kwa wakati.
- (vi) Kufanya utatuzi wa miamala kwa mujibu wa idhini na kwa kuzingatia busara na udhibiti uliopo wa ndani ya Chama.
- (vii) Kutayarisha taarifa za kisheria na udhibiti kulingana na viwango vinavyokubalika vya uhasibu;
- (viii) Kutoa mwongozo kwa Menejimenti kuhusu masuala yanayohusu uhasibu pamoja na utoaji wa taarifa za fedha na udhibiti;
- (ix) Kutekeleza majukumu mengine kama ilivyoelekezwa na msimamizi wake yanayoendana na kazi yake.

## **MTUNZA KUMBUKUMBU 'RECORD MANAGEMENT' (NAFASI 1).**

### **VIGEZO NA UZOEFU.**

- I. Muombaji awe na Stashahada ya Utunzaji kumbukumbu kutoka chuo kinacho tambuliwa na Serikali.
- II. Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili.
- III. Awe ni raia wa Tanzania.
- IV. Awe na Umri wa kuanzia miaka 25 na kuendelea.
- V. Awe hajawahi kuhukumiwa kwa kosa la jinai.
- VI. Awe na uwezo wa kutumia Compyuta.

## **MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

- I. Kutafuta kumbukumbu/Nyaraka/Majalada yanayohitajiwa na Wasomaji.
- II. Kudhibiti upokeaji, Uandikishaji wa Kumbukumbu/ Nyaraka.
- III. Kuchambua, Kuboresha, na Kupanga kumbukumbu/Nyaraka/Majarada katika Makundi kulingana na somo husika kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- IV. Kuweka, kupanga kumbukumbu/Nyaraka, katika reki katika Masijala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- V. Kuweka Kumbukumbu (Barua, Nyaraka muhimu n.k) katika majalada.
- VI. Kupokea Nyaraka za kiofisi.
- VII. Kufanya Shughuli nyinginezo atakazoelekezwa na Uongozi.

## **AFISA UBORA & MUONJAJI WA KAHAWA (NAFASI 1).**

- I. Awe na Stashahada ya Kilimo/Ubora/ toka chuo kinachotambuliwa na Serikali, Mwenye Cheti cha Uonjaji wa Kahawa atakuwa ana sifa ya ziada.
- II. Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili.
- III. Awe ni raia wa Tanzania.
- IV. Awe na Umri wa kuanzia miaka 25 na kuendelea.
- V. Awe hajawahi kuhukumiwa kwa kosa la jinai.
- VI. Awe na uwezo wa kutumia Compyuta.

## **MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

- (i) Kuhakiki ubora wa kahawa.
- (ii) Kuhakiki muonjo mzuri wa kahawa.
- (iii) Kuandaa sampuli za kahawa na kuziwasilisha mnadani.
- (iv) Kukaanga na kusaga Kahawa ya uonjaji kabla ya mnada.
- (v) Kutunza nyaraka na taarifa za sampuli na uonjaji.
- (vi) Kuandaa na kutuma sampuli kwa wateja wa ndani na nje ya nchi.
- (vii) Kufanya kazi nyinginezo kama zitakavyoelekezwa na kiongozi wake.

## **MAMBO MUHIMU KWA UJUMLA.**

**MSHAHARA:** Ni kulingana na viwango vya Mshahara vya KCU (1990) LTD.

## **VIAMBATISHO.**

Kwa kila muombaji anatakiwa kutuma;

- Barua ya maombi ya kazi iliyosainiwa ikiambatana na Nakala ya cheti cha kuzaliwa na vyeti vya elimu ya Sekondari, pamoja na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria.
- Wasifu binafsi (CV).
- Picha ndogo moja pamoja na
- Majina na anwani za wadhamini wake watatu (3).

Barua zote za maombi ya kazi ziandikwe kwa;

**Meneja Mkuu,  
KCU (1990) LTD,  
SLP 5,  
BUKOBA.**

**NB.** Mwisho wa kupokea barua za maombi haya ya kazi ni tarehe 08/Februari/2025. Ifikapo saa 4:00 kamili asubuhi.

*....Ajira Mpya KCU (1990) LTD....*